

BARAZA LA TAIFA LA HIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA

Simu: 022 2774889
Nukushi: 022 2774901
Tovuti: www.nemc.or.tz
Barua pepe: dg@nemc.or.tz



35 Mtaa wa Regent,
S.L.P 63154
11404 Dar es Salaam
TANZANIA.

TAARIFA KWA UMMA

MAPAMBANO DHIDI YA HOMA KALI YA MAPAFU INAYOSABABISHWA NA VIRUSI VYA CORONA (COVID-19)

Dar es Salaam, Aprili 21, 2020

Kufuatia tamko la Serikali kuhusu kuchukua tahadhari dhidi ya kuenea kwa ugonjwa wa homa kali ya mapafu unaosababishwa na virusi vya Corona (Covid-19) hapa nchini, Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) linatoa maelekezo yafuatayo kwa wadau na wananchi kiujumla ;

Kuanzia **Jumane tarehe 21 Aprili, 2020** Wananchi na wadau wote watakaofika katika ofisi za NEMC watalazimika kuvaa Barakoa (face masks), pia wanapaswa kuzingatia taratibu zote za kiafya zilizowekwa katika ofisi zetu ikiwemo kunawa mikono kwa sabuni au kutumia vitakasa mikono (sanitizers) vilivyowekwa kabla ya kuingia katika ofisi husika na wakati wa kutoka.

Tunawashauri wananchi kutumia mawasiliano ya simu na barua pepe kwa masuala yasiyo ya lazima kufika ofisini ili kupunguza msongamano.

NEMC inaendelea kuchukua hatua zote muhimu za tahadhari dhidi ya ugojwa wa Covid-19 bila kuathiri utendaji wake na utoaji huduma kwa wananchi na wadau wetu.

Baraza linawashukuru sana kwa ushirikiano wenu na linawatakia kila la kheri katika mapambano haya.

- NEMC Makao Makuu
Simu: +255 22 27744852/4889
Barua pepe: dg@nemc.or.tz
- Kanda ya Nyanda za Juu Kusini
Simu: +255 737796253
Barua pepe: nemcmbeya@nemc.or.tz

- Kanda ya Kaskazini
Simu: +255 738064966
Barua pepe: nemcarusha@nemc.or.tz
- Kanda ya kati
Barua pepe: nemcdodoma@nemc.or.tz
Simu: +255 262963859
- Kanda ya Kusini
Simu: +255 232334683
Barua pepe: nemcmtwara@nemc.or.tz
- Kanda ya Magharibi
Simu: +255 738037307
Barua pepe: nemckigoma@nemc.or.tz
- Kanda ya Ziwa Victoria
Simu: +255 737988999
Barua pepe: nemcmwanza@nemc.or.tz

Kwa Pamoja Tutaitokomeza Corona Tanzania!

Imetolewa na :



Johary Kachwamba

Meneja Uhusiano na Mawasiliano

NEMC Makao Makuu